



JINA \_\_\_\_\_

NAMBAJI YAKO \_\_\_\_\_

DARASA \_\_\_\_\_

102/3

KISWAHILI

FASIHI

MUDA: SAA 2 ½

**SHULE YA UPILI YA LLAINACE  
MTIHANI WA MWIGA – MIGO KIDATO CHA NNE 2016**

**MAAGIZO**

1. Jibu maswali manne pekee
2. Swali la kwanza ni la lazima
3. Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kitoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadhithi Fupi, na Fasihi Simulizi.
4. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
5. Kila swali lina alama 20

### **SEHEMU A: USHAIRI (AL 20 ) SWALI LA LAZIMA**

- a) Angawa mdongo, amekomaa  
Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa  
Kalia kiriaya, dagaa, h'ondoa njaa
- Wa kwako udogo, kijana sio balaa  
Na sio mzigo, kijana, bado wafaa  
Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa
- Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa  
Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa  
Chinbung'aa, kijana, usibung'aa
- Na wake udogo, dagaa, ndani hukaa,  
Kuliko vigogo, dagaa, ambaa  
Hapati kipigo, dagaa, hakuna fazaa
- Maisha si mwigo, kijana ushike taa  
Sihofu magego, kijana, nawe wafaa  
Kazana kidog, kijana, kugaaga

### **b) Siafu wamekazana**

Nyoka amegutuka, ndani ya shimo kutuna,  
Tena amekasirka, hasira zenyenununa,  
Nyoka anababaika, shimonii kwa kujikuna,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Shimoni atacondoka, hilo nataja kwa jina,  
Nyoka anajuwa fika, siafu wakiungana,  
Nguvu zao zaongezeka, shimonii watagomana,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Siafu wakijishika, mshiko kushikamana.  
Kwamba wanampeleka, sultani wao bwana,  
Shimoni wanapofika, nyoka la kufanya hana,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Siafu wanapofika, na nyoka wakikutana,  
Nyoka haweziz kufoka, huwa ametulizana,  
Ndipo nyoka huondoka, na wana wakilizana,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika

Kupo na kukanganyika, hilo na natujue sana,  
Nyoka anapoondoka, siafu hulaliana,  
Hiuma hupumzika, hapo hakutafanana,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika.

Nyoka akishaondoka, na siafu hujazana,  
Shimoni wakipeleka, vyakula kutiliana,  
Ndilo walilotaka, wale kwa kutulizana,  
Siafu wamekazana, nyoka amekasirika  
(S. Abdu Kandoro)

- a) Kwa Kuzingatia vigezo vifuatavyo bainisha bahari za mashairi yote mawili ( alama 2)
- b) Eleza toni katika mashairi haya. ( alama 2)
- c) Bainisha matumizi ya mbinu zifuatazo
  - i) Methali
  - ii) IstiariKatika shairi (a)
- d) Andika ubeti wa sita wa shairi (b) kwa lugha ya nathari. ( alama 2)
- e) Onyesha umuhimu wa kibwagizo katika shairi (b) ( alama 2)
- g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kutokana na washairi
  - i) Nyoka hawezi kufoka
  - ii) Sihofu magego
- h) Tamibia nafsi neni katika mashairi haya. ( alama 2)

#### SEEEMU YA B RIWAYA

Kidagaa Kimemwozoa, Ken Walibora.

- 2. a) Ajabu hino ajabu, ya nyangumi kufa maji.....  
Alokuwa ni hatibu, ameshauma maji.....  
Aliyekuwa hanacho, hana anachotamani.....
    - i) Eleza muktadha wa maneno hayo (alama 2)
    - ii) Huku ukirejelea kila mshororo taja wahusika wanaorejelewa na maneno hayo. (alama 4)
  - b) Kwa kurejelea mbinu zifuatazo, taja mifano ya matumizi yake katika riwaya husika.
    - i) Nyimbo (alama 6)
    - ii.) Barua (alama. 8)
- 3" Wenzake wa kirimu yake walikihuudu kwa umahiri wake wa Kiswahili hicho cha pekee, aina ya Kiswahili kisemwacho sana mijini na majijini?"
- a) i) Eleza muktadha wa maneno haya. ( alama 4)
  - ii) Taja sifa za mhusika anayerejelewa. ( alama 8)
  - b) Katika jamii ya Kidagaa Kimemuozea, Lugha ya Kiswahili imekumbwa na vizingiti vya kukua kwake. Dhibitisha kauli hii kwa kutoa mifano mwafaka. (alama 8)

**SEHEMU YA C : TAMITHILIA**  
**MSTAHIKI MEYA: Timothy Aregå.**

4. "Sikio la Kufa haliskii dawa" Thibitisha ufaafu wa methali hii huku ukirejelea tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 20)
5. "Ndugu Meya, tumetumwa na makao makuu kuwachukua mwenda kueleza mbele hali hii ya mambo.
- a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)
  - b) Taja na ulezea sifa za msemaji wa maneno haya na asasi anayoiwasilishaa (alama 4)
  - c) Kwa kurejelea tamthilia husika, thibitisha kuwa tukio linalohusika katika muktadha huu ni kinaya, linapolinganisha na sifa za mstahiki Meya. (alama 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI: NYEUSI NA HADITHI NYINGINE**

6. Aje hapa!  
Tunangaike naye!  
Eeh aje hapa!
- a) Eleza muktadha wa dondo hili (alama 4)
  - b) Fafanua mbinu mbili za kimtindo zilizotumika katika dondo hili. (alama 2)
  - c) Eleza mambo saba yaliyokuwa yakimhangainsha anayezungumziwa. (alama 14)
7. "Nyumbani ni nyubani ingawa pangoni,"
- i) Eleza muktadha wa dondo hili. (alama 4)
  - ii) Jadili ufaafu wa methali hii ukimrejelea mhusika. (alama 10)
  - iii) Taja na ufanue sifa tatu za mhyuzika anayerejelewa. (alama 6)

**SEHEMU E – Fasihi Simulizi (alama 20)**

8. a) Eleza maana ya misimu (alama 2)
- b) Kwa kutolea mifano minne onyesha jinsi misimu inavyoundwa (alama 8)
- c) Methali ni nini? (alama 2)
- d) Huku ukitoa mifano jadili mbinu nne za kimtindo za methali. (alama 8)